Desire To Change for The Positive Results

# HYPERLINK SCHOOLS OF TANZANIA (HSoT)

## SHULE YA CHEKECHEA, AWALI NA MSINGI

## FALSAFA YA SHULE

*"Elimu Bora na Jumuishi kwa Gharama Nafuu"*

## FOMU YA MAOMBI YA KUJIUNGA NA SHULE

## MWAKA 2025/2026


**Mawasiliano:**

Mkuu wa Shule: 0754-505-598
Ofisi ya Meneja: 0767-030-406
Barua Pepe: info@hyperlinkschools.ac.tz
Tovuti: www.hyperlinkschools.ac.tz

**S.L.P: 345**
**IRINGA**


**NAMBA YA FOMU:**

**HSoT:...................**

## IFAHAMU SHULE YA HYPERLINK

### HISTORIA YA SHULE

Shule ya Hyperlink ilianzishwa kwa lengo la kupunguza changamoto ya lugha ya kiingereza kwa mwanafunzi anaye hitimu elimu ya msingi na kujiunga na elimu ya sekondari. Shule za awali na msingi nyingi za serikali, elimu itolewayo ni kwa lugha ya Kiswahili isipo kuwa kiingereza ambacho hufundishwa kama somo kwa hatua ya darasa la tatu.

Wazo la kuanzisha shule limekuwepo mara baada ya kujiunga na elimu ya sekondari wakati huo ukitokea shule za msingi za kawaida za serikali ambapo msingi wa lugha ya kiingereza umekuwa hafifu sana na kunipatia changamoto kuanza elimu yangu ya sekodari ambapo masomo yote hufundishwa kwa lugha ya kiingereza isipokuwa somo la Kiswahili tu.

Ilinipasa nijifunze kiingereza kwa ari na nidhamu kubwa ambapo ilipelekea kutumia muda mwingi kujifunza vitu vingi kwa wakati mmoja na kutokuwa na matokeo mazuri sana kwa hatua ya kidato cha kwanza na kwasababu hiyo, nilipata wazo la siku moja katika maisha yangu nije kuanzisha shule itakayokuwa ya mchepuo wa lugha ya kiingereza ili kuwa jengea misingi bora wanafunzi wa chekechea, awali na msingi wenye umri wa kwenda shule.

kuweza kutimiza adhma hii, niliamua kusomea uwalimu kwa ngazi ya stashahada na shahada ya elimu ya juu ili nije kutekeleza kwa vitendo maono niliyokuwa nayo ya kuanzisha shule.

Nilipata msukumo mkubwa wakati nafanya kazi serikalini bado niliweza kuona changamoto ya kiingereza kwa wanafunzi niliokuwa nikiwafundisha somo la Hesabu na Sayansi na hapa ikanipatia uwanja mpana wa uelewa wa tatizo.

Wakati huo nilifanikiwa kuanzisha kituo cha kuwajengea wanafunzi wa shule za msingi, misingi ya lugha ya kiingereza na hesabu na kufanikiwa kuajiri walimu wenzangu ambao waliweza kufundisha katika muda wa ziada na wakati wa mwisho wa wiki.

Na mwezi wa kumi mwaka **2010** shule ya Hyperlink ilianzishwa kama kituo cha twisheni kwa wanafunzi wa shule ya msingi na sekodari hadi mwaka **2011**, ikaanzishwa chekechea na baadae usajili wa shule ya awali na msingi mwezi wa kumi na mbili mwaka **2016** na kupata **usajili wa shule** ya **Hyperlink ya kutwa** na **bweni** kwa usajili wenye namba ya usajili **EM.17709**

### MAHALI SHULE INAPATIKANA

Shule ya C**hekechea**, **Awali** na **Msingi** ya Hyperlink ya mchepuo wa lugha ya kiingereza, inapatikana umbali wa kilomita tisa **(9)** ukitokea kwenye Mnara wa saa wa Manispaa ya Iringa. Ukifuata barabara inayoelekea **Mkwawa chuo** na pia

mkabala na barabara ya Pawaga, mtaa wa Hoho (Itamba), kata ya Mkwawa, Manispaa ya Iringa, Mkoa wa Iringa.

Unaweza kuifikia shule ya Hyperlink, kwa kupanda dala dala za Mkwawa - Kiwele, bajaj au pia waweza kuifikia shule kwa kutumia usafiri wa boda boda. Waweza kuitembelea shule kwa kutumia usafiri wako binafsi ni karibu sana.

**MANDHALI YA SHULE ILIPO**

Shule imeweza kukidhi miundo mbinu ya msingi kwa jamii yake yote (wanafunzi, wafanyakazi na wageni pamoja na jamii inayoizunguka shule), shule ina majengo ya kisasa kuanzia ofisi, madarasa yenye kupitisha hewa ya kutosha, mabweni yenye vyumba safi na vimefungwa vifaa viashiria moto, ukumbi wa mikutano, mabanda ya mifugo, bembea za kutosha za wanafunzi, viwanja vya michezo, bustani za mboga mboga, bara bara safi na salama ndani ya shule, barabara inayopitika kwa mwaka mzima kwa mabasi ya shule na wadau wa shule, uwepo wa maji ya bomba na maji ya kisima, umeme wa Tanesco, mtandao (internet), maktaba, bustani ya maua na miti ya kimvuli.

Shule inazungukwa na milima inayovutia ambayo inauoto wa asili unaohifadhiwa ambapo unapelekea kuwavutia wanafunzi na wafanyakazi pindi wakiwa kwenye mapumziko au kutekeleza majukumu yao mbali mbali ya kila siku. Nyakati za usiku kunakuwa na mwonekano mwanana wa taa zinazomelemeta kutokea katikati ya Manispaa ya Iringa kusini mashariki mwa shule ya Hyperlink. Hiki ni kivutio kikubwa na cha tofauti cha kumsababisha mwanafunzi ahisi utofauti na aweze kuzingatie masomo.

Ni shule pekee inayopatikana katika kata na chuo kwa pamoja zinabeba jina muhimu la shujaa wa wahehe na mbabe wa wakoloni "**MKWAWA**"

**USALAMA WA MWANAFUNZI AWAPO NDANI NA NJE YA SHULE**

Msingi mkubwa wa shule ya Hyperlink umejengeka kwenye **NIDHAMU**, kama shule tunaamini kila kitu kinawezekana ikiwa nidhamu itapewa kipaumbele.

Nidhamu kwetu huanzia kwenye uongozi wa shule na kwenda kwa kila mfanyakazi na kuishia kwa kila mwanafunzi, hapa tunautaratibu mzuri wa kudumisha nidhamu kwa kuzingatia kila lalamiko ambalo litakuwa limewekwa kwenye **Sanduku la Maoni** na huchukuliwa hatua stahiki ikiwemo wale wanao lalamikiwa kuvunja nidhamu, huitwa na kukarishwa kwenye vikao vya nidhamu na vikao hivi vimekuwa vikitoka na maadhimio kadha wa kadha ambapo mkosaji anabadilishwa mwenendo wa tabia na kufuata sheria na taratibu za shule.

**MISINGI YA IMANI/ DINI**

Shule ya Hyperlink inaheshimu na kulinda kwa kusimamia misingi ya kuabudu kwa kila mwanafunzi na mfanyakazi kwa Imani yake.

Nidhamu hujengwa kwa kila mdau wa shule kwa kufuata misingi ya Imani yake, japo shule inautaratibu pekee wa kufanya ibada ya pamoja kila siku

kabla ya kuanza masomo na kwa wanafunzi wa bweni wanafanya hivyo kabla ya kwenda kusoma muda wa usiku.

Tuna kipindi kimoja katika juma kwa walimu wa dini kuja shule na kuwafundisha wanafunzi misingi ya Imani husika na hili limetusaidia sana kuwajengea wanafunzi nidhamu bora

Wanafunzi wa kiislamu wanashiriki ibada msikitini siku ya Ijumaa na wanapelekwa na usafiri wa shule na kwa madhebu mengine ya kikristo wanashiriki ibada siku ya Jumamosi na Jumapili kwa makanisa husika. Tunajipanga kuboresha usafiri kwa wanafunzi wa bweni wanao kwenda kanisani kwa siku za Jumamosi na Jumapili.

**Wanafunzi** kupewa elimu ya uelewa wa sheria na taratibu za shule kikamilifu hii huwasaidia kufahamu nini cha kufanya na kipi si cha kufanya

**Mwanafunzi wa bweni** tunahakikisha anafuata ratiba kamili ya kila siku (**Daily Routine**) ambapo muda wote anapaswa kuwa sehemu sahihi na kufanya jambo lililopangwa kwenye ratiba ya shule

**Mwanafunzi wa kutwa anayetumia usafiri,** kwa usalama wao ndani na nje ya Basi la shule tunao walezi wa wakike ambapo jukumu lao ni kuangalia usalama wa wanafunzi wawapo ndani ya usafi na kuwavusha na kuwapakia Katika vituo husika. Madereva wenye leseni ya **daraja C** kama inavyohitajika na mamlaka husika na wakati wote hupaswa kuzingatia sheria za matumizi sahihi ya bara bara.

**ELIMU/ TAALUMA:**

Falsafa ya shule ya Hyperlink ni kutoa Elimu Bora na Jumuishi kwa Gharama Nafuu, ili kuwawezesha Watoto wengi wenye umri wa Kwenda shule waweze kupata fursa hii muhimu katika maisha yao.

A. **Elimu ya Darasani**

   Kwa kuzingatia falsafa ya shule, shule inasimamia Programu Maalum ya namna bora ya kuwapata wafanyakazi wa shule na kuwajengea uwezo wa mara kwa mara ili kuendana na falsafa ya shule yetu. Kupitia uelewa wa falsafa ya shule yetu, mwanafunzi anajengewa **UMAHIRI** katika misingi mitano ya ujifunzaji ambayo ni: - **Kusikiliza**, **Kufikiri**, **Kuandika**, **Kusoma** na **Kuhesabu**

## MATOKEO YA MITIHANI YA KITAIFA DARASA LA VII KWA MIAKA MITATU (3) MFULULIZO 2022, 2023 NA 2024

| MWAKA | A | B | C | D | E |
|---|---|---|---|---|---|
| 2024 | 19 | 2 | 0 | 0 | 0 |
| 2023 | 12 | 21 | 2 | 0 | 0 |
| 2022 | 29 | 7 | 1 | 0 | 0 |

## WANAFUNZI WALIOCHAGULIWA SHULE ZA VIPAJI MAALUM KWA MIAKA MITATU MFULULIZO 2022, 2023 NA 2024

| MWAKA | ALAMA YA UFAULU | IDADI YA WANAFUNZI WALIOCHAGULIWA KWENDA SHULE ZA VIPAJI MAALUMU |
|---|---|---|
| 2024 | DARAJA A (BORA) | 3 |
| 2023 | DARAJA B (NZURI SANA) | - |
| 2022 | DARAJA A (BORA) | 1 |

**Matokeo haya yamepatikana bila kuchuja mwanafunzi yoyote**

**B. Elimu ya Kujitegemea**

Kila mara shule imekuwa ikifanya utafiti juu ya changamoto zinazo ikabili jamii yetu zilizopo ndani na nje ya shule kwa lengo la kuboresha na kujifunza misingi ya changamoto hizo.

Ndugu mzazi / mlezi utakubaliana nasi kuwa kipimo cha elimu itolewayo imekuwa ni **ufaulu tu wa darasani**, mwanafunzi anaweza kuwa na ufaulu mkubwa lakini ukimleta kwenye mazingira ya Maisha ya mtaani, kijana anashindwa kukabililana na changamoto za Maisha kwa kukosa misingi bora ya kumwezesha **kujitegemea**. Na vijana wengi wameshindwa kuwa wabunifu na badala yake wameendelea kuwa tegemezi katika familia na Taifa.

Baada ya kulitambua hilo, shule imekuwa ikitekeleza mpango maalum unao julikana kama **JINASUE KATIKA MAISHA,** huu mpango unawasaidia wanafunzi kuanzia ngazi ya **chekechea** kuweza kupunguza changamoto ya kukosa ajira na kushindwa kuwa wabunifu:

**MKAKATI WA JINASUE KATIKA MAISHA**

1. Kufundisha mwanafunzi namna sahihi ya kufikiri na kutafiti kupitia midahalo mbali mbali ndani ya shule ili kuweza kubainisha vipaumbele vya kila mwanfunzi katika Maisha, pamoja na kutambua fursa zilizopo.
2. Mpango endelevu wa machaguo ya ujuzi hitajika (Sustainable Career Development Program) ambapo kila mwanafunzi atakuwa amechagua au kushauriwa na walimu au wazazi wake.

3. Uwepo wa ratiba rafiki itakayosaidia kutekeleza machaguo ya ujuzi katika uhalisia wake.
4. Mafunzo kwa vitendo, ambapo kila mwanafunzi atatakiwa kuwa na shughuli nyumbani ya kutekeleza na kusimamia kulingana na machaguo yake.
5. Ufuatiliaji na usimamizi utafanyika chini ya walimu wa miradi husika, wanafunzi na wazazi.
6. Ufanyikaji wa tathmini ya kila robo mhula kuweza kujifunza maendeleo, mafanikio na changamoto zitokanazo na mpango husika.

Baadhi ya maeneo ambayo wanafunzi na walimu wameweza kuyabainisha ili kutekeleza Elimu ya kujitegemea kwa vitendo na tumeanza na maeneo machache ili tuweze kuyasimamia vyema.

- **Taaluma ya Michezo**
  Wanafunzi hufundishwa taaluma ya michezo (**Sport Academy**) kama sehemu ya kuimarisha afya za wanafunzi, kuwajengea ukakamavu, mshikamano, upendo, kujiamini na kuboresha afya ya utimamu wa Akili. Pamoja na kutumia kama fursa ya ajira kwa siku za baadaye.
- **Kilimo na Ufugaji**
  Shule inafuga ng'ombe wa maziwa, mbuzi, kuku, bustani za mboga na matunda kwa wanafunzi kupata stadi za maisha na chakula.
  Na baadhi ya wanafunzi wetu wameanza kufuga kuku majumbani kwao ili kuendeleza ujuzi walioupata shuleni.
- **Mafunzo ya Kompyuta**
  Kwa dunia ya sasa na kesho shule yetu imeonelea ni vyema kuanza mapema kuwafundisha wanafunzi ujuzi wa **kompyuta** katika maeneo kadhaa kama vile: Ugunduzi wa matatizo ya Kompyuta, matengenezo yake (Computer Diagnosis, Maintenance and Repair), Utengenezaji wa mifumo ya kompyuta (Software Development), Ujuzi wa Akili Mnemba (Artificial Intelligence), Ujuzi wa ulinzi wa kompyuta na mifumo ya kompyuta (Computer Security and Cyber Crime), Usanifu michoro na picha mjongeo kwa kutumia Kompyuta (Computer Ghaphics Design and Multmedia).
- **Uelewa wa Elimu ya fedha (Financial Literacy)**
  Kuwafundisha wanafunzi uelewa kuhusu elimu ya fedha na Uchumi.

**Lengo la shule ni kuweza kuibua na kuendeleza UJUZI mbali mbali kwa wanafunzi wetu ili kuwaandaa vyema na ushindani katika soko la ajira na maisha kwa ujumla.**

C. **Elimu Rika (Elimu ya Kujitambua)**
Changamoto ipo katika jamii zetu hasa kwa upande wa kujitambua, shule ya Hyperlink inaweka mkazo mkubwa katika kuwajengea wanafunzi wake uelewa wa elimu ya kujitambua
- Afya binafsi
- Tabia binafsi
- Umuhimu wa kuishi

**MAONO YA SHULE YA HYPERLINK:**
Kutoa Elimu Bora

**DHAMIRA YA SHULE YA HYPERLINK:**
Kuhakikisha kila Mwanafunzi ameelimika na anajitambua

**TUNU ZA SHULE:**
1. Elimu bora
2. Uwajibikaji
3. Nidhamu
4. Uwazi
5. Utu
6. Ushiriki

**MUUNDO WA UONGOZI WA SHULE YA HYPERLINK:**
- Mkurugenzi wa shule-Anabeba maono ya shule
- Kamati ya shule-Kushauri uongozi wa shule na kusimamia shule
- Kitengo cha manunuzi-Kusimamia manunuzi ya mahitaji ya shule
- Mkuu wa shule – Msimamizi mkuu wa shughuli zote za shule za kila siku
- Mwangalizi wa ofisi – Husimamia ofisi katika utendaji wake wa kila siku
- Mkuu wa Idara ya Taaluma- Mtendaji mkuu wa taaluma kwa wanafunzi na walimu
- Mratibu wa shule- Husimamia miradi na elimu ya kujitegemea
- Mhasibu wa shule – Husimamia mapato na matumizi ya shule na utawala

HYPERLINK SCHOOLS OF TANZANIA

SCHOOL'S ORGANIATIONAL STRUCTURE




Kwa Falsafa ya shule yetu, tunazingatia sana elimu ya darasani, kujitambua na elimu ya kujitegemea kwa mwanafunzi na mfanyakazi kwa pamoja. Hivyo, uongozi wa shule wakati wote unasimamia **NIDHAMU** kwa mwanafunzi na mfanyakazi.

## SHERIA KUU ZA SHULE

1. Wanafunzi wote wanapaswa kuheshimu na kutii sheria zaJamhuri yaMuungano wa Tanzania.
2. Wanafunzi wote wanapaswa kutii na kuheshimu Uongozi na Mamlaka zote za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Shule na Jamii.
3. Wanafunzi wote wanapaswa kutii na kufuata taratibu za kila siku za uendeshaji wa shule, bila ya kujali itikadi za dini zao.
4. Wanafunzi hawaruhusiwi kuhodhi fedha na vyakula nje ya utaratibu uliowekwa.
5. Wanafunzi wote wanapaswa kutunza mali zao binafsi, mali za shule na mali za umma na mazingira kwa ujumla.
6. Wanafunzi wote wanapaswa kujitahidi na kufikia viwango vya ufaulu wa masomo vilivyowekwa na shule.
7. Mwanafunzi anapaswa kuhudhuria siku zote shuleni, kukosa kuhudhuria shule kwa siku **14** kwa muhula itapelekea kusitishiwa usajili.
8. Mwanafunza anapaswa kufanya mitihani yote inayoandaliwa na shule. Kutofanya mtihani wowote wa shule au kufanya udanganyifu wowote

kwenye mtihani ni kosa ambalo litapelekea kusitishiwa usajili mara moja.

9. Kila mzazi/ mlezi anawajibika kutii na kufuata taratibu zilizowekwa na shule na kutoa ushirikiano ili kufikia malengo ya wanafunzi na shule kwa ujumla

**NB**: Kushindwa kufuata na kutii sheria kuu za shule (kuanzia 1-9) kutasababisha kufutiwa usajili wa mwanafunzi husika.

**KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE**

Kanuni na taratibu za shule yetu zinalenga kuwaongoza watu kuishi kwa amani, utulivu na kufuata utaratibu wa shule ili kutimiza malengo ya mwanafunzi kitaaluma na kuishi kistaarabu. Mwanafunzi atakayekiuka kanuni hizi atachukuliwa hatua za kinidhamu na taarifa zake zitaandikwa kwenye kumbukumbu za shule, pamoja na jalada la mwanafunzi. Mwanafunzi atakayeshindwa kufuata kanuni na sheria za shule anahatarisha amani na utulivu kwa jamii ya shule; kwa sababu hiyo atashauriwa atafute shule nyingine bila kurejeshewa karo (ada) aliyolipa .

1. **RATIBA YA SHULE:**
   Kila mwanafunzi anatarajiwa kuwepo mahali sahihi kwa wakati sahihi. Mwanafunzi asiyehudhuria mahali husika atapewa adhabu na endapo atashindwa kubadilika, mzazi atashauriwa atafute shule nyingine. Aidha shule yetu inafanya kazi siku sita za juma, Jumatatu hadi Jumamosi.

2. **MAWASILIANO:**
   a. Lugha ya kufundishia shuleni wakati wote ni kiingereza isipokuwa kwa somo la Kiswahili na vipindi vya dini. Wanafunzi wanatakiwa kutumia lugha ya kiingereza muda wote ili kuboresha uwezo wao wa kujieleza. Kutumia lugha tofauti na kiingereza ni kosa
   b. Matumizi ya Lugha chafu na ishara zisizo na staha hazitavumiliwa kabisa shuleni. Mwanafunzi atakayetumia lugha chafu au ishara zisizo na staha atapewa adhabu, akirudia atarudishwa nyumbani.

3. **MIPAKA YA KIJINSIA:**
   Mara zote mwanafunzi awapo shuleni ni lazima kuzingatia mipaka ya kijinsia kati ya Mvulana na Msichana hata kwa wafanyakazi pia. Wakati wa masomo ya darasani na hata baada ya masomo mipaka ya kijinsia izingatiwe.

4. **MALI BINAFSI:**

   Ni wajibu wa kila mwanafunzi kutunza mali zake mwenyewe kama vitabu, nguo, mashuka n.k Atakayeshindwa kutunza mali zake

atapewa adhabu ili kumkumbusha wajibu wake. Aidha mali zote za mwanafunzi zinapaswa kuandikwa majina yake kwa maandishi yatakayoonekana wazi. Mfano: kudarizi jina kwenye nguo na mashuka kwa maandishi makubwa.

5. **MALI ZA SHULE:**

   Mwanafunzi atakabidhiwa vifaa vyake vya kutumia awapo shuleni kama dawati, kiti, kitanda na vinginevyo. Mwanafunzi anatakiwa avitumie vizuri na asivipoteze au kuviharibu. Kifaa chochote kitakachopotea au kuharibika, mzazi/mlezi wake atawajibika kulipa mara moja.

   a. Pia ni marufuku kuandika kwenye ukuta, madawati, kiti, meza au kwenye miti.
   b. Uharibifu wa makusudi wa mali na mazingira ya shule utapelekea kusitishiwa usajili mara moja.

6. **RUHUSA ZA KUTOKA NJE YA SHULE:**

   a. Mwanafunzi haruhusiwi kabisa kutoka nje ya mipaka ya shule bila kibali maalumu. Atakayekiuka atafutiwa usajili wake mara moja.

   b. Mwanafunzi atakayeruhusiwa kutoka nje ya shule ni lazima avae sare ya shule wakati wa kutoka na kurudi shuleni. Pia atatakiwa arudi shuleni kwa wakati uliopangwa. Atakayekiuka atapewa adhabu na mzazi/mlezi wake atatakiwa kutoa maelezo.

   c. Mwanafunzi haruhusiwi kabisa kutembelea sehemu zifuatazo bila kibali maalum.

   - Jikoni, Nyumba za wafanyakazi, Maktaba na Ofisi za walimu

7. **SARE ZA SHULE:**

   a. Wakati wote mwanafunzi awapo shuleni atapaswa avae sare rasmi ya shule. Atakayekiuka atapewa adhabu na nguo zisizo rasmi zitaharibiwa.
   b. Baada ya masomo mwanafunzi ataruhusiwa kuvaa sandals akiwa maeneo ya madarasani au jikoni. Sandals zinazotakiwa sio za matairi ya gari au pikipiki wala ndala. Siku za wiki-end watavaa T-shirts na shamba dress na sandals nzuri au viatu.
   c. Sare zikichakaa, mzazi atagharamia kununua zingine.

8. **USAFI:**

   a. Mwanafunzi wa kiume haruhusiwi kufuga nywele, ndevu au kucha. Pia hapaswi kuvaa hereni, pete, mkufu, culture threads, bangili za aina zote au kunyoa kwa mitindo ya mitaani.

   b. Wasichana watapaswa kusuka mtindo wa nywele tano (twende kilioni), au kunyoa na kuwa na nywele fupi. Pia hawapaswi kuvaa hereni, pete, mkufu, culture, bangili, kufuga kucha, kupaka rangi kucha au urembo wa aina yeyote.

atapewa adhabu ili kumkumbusha wajibu wake. Aidha mali zote za mwanafunzi zinapaswa kuandikwa majina yake kwa maandishi yatakayoonekana wazi. Mfano: kudarizi jina kwenye nguo na mashuka kwa maandishi makubwa.

5. **MALI ZA SHULE:**

   Mwanafunzi atakabidhiwa vifaa vyake vya kutumia awapo shuleni kama dawati, kiti, kitanda na vinginevyo. Mwanafunzi anatakiwa avitumie vizuri na asivipoteze au kuviharibu. Kifaa chochote kitakachopotea au kuharibika, mzazi/mlezi wake atawajibika kulipa mara moja.

   a. Pia ni marufuku kuandika kwenye ukuta, madawati, kiti, meza au kwenye miti.
   b. Uharibifu wa makusudi wa mali na mazingira ya shule utapelekea kusitishiwa usajili mara moja.

6. **RUHUSA ZA KUTOKA NJE YA SHULE:**

   a. Mwanafunzi haruhusiwi kabisa kutoka nje ya mipaka ya shule bila kibali maalumu. Atakayekiuka atafutiwa usajili wake mara moja.

   b. Mwanafunzi atakayeruhusiwa kutoka nje ya shule ni lazima avae sare ya shule wakati wa kutoka na kurudi shuleni. Pia atatakiwa arudi shuleni kwa wakati uliopangwa. Atakayekiuka atapewa adhabu na mzazi/mlezi wake atatakiwa kutoa maelezo.

   c. Mwanafunzi haruhusiwi kabisa kutembelea sehemu zifuatazo bila kibali maalum.

   - Jikoni, Nyumba za wafanyakazi, Maktaba na Ofisi za walimu

7. **SARE ZA SHULE:**

   a. Wakati wote mwanafunzi awapo shuleni atapaswa avae sare rasmi ya shule. Atakayekiuka atapewa adhabu na nguo zisizo rasmi zitaharibiwa.
   b. Baada ya masomo mwanafunzi ataruhusiwa kuvaa sandals akiwa maeneo ya madarasani au jikoni. Sandals zinazotakiwa sio za matairi ya gari au pikipiki wala ndala. Siku za wiki-end watavaa T-shirts na shamba dress na sandals nzuri au viatu.
   c. Sare zikichakaa, mzazi atagharamia kununua zingine.

8. **USAFI:**

   a. Mwanafunzi wa kiume haruhusiwi kufuga nywele, ndevu au kucha. Pia hapaswi kuvaa hereni, pete, mkufu, culture threads, bangili za aina zote au kunyoa kwa mitindo ya mitaani.

   b. Wasichana watapaswa kusuka mtindo wa nywele tano (twende kilioni), au kunyoa na kuwa na nywele fupi. Pia hawapaswi kuvaa hereni, pete, mkufu, culture, bangili, kufuga kucha, kupaka rangi kucha au urembo wa aina yeyote.

c. Kwa wanaovaa hijabu wanapaswa kuvaa hijabu ya rangi nyeupe tu wakati wote.

d. Usafi binafsi, mabwenini, madarasani na mazingira ya shule unafanywa na wanafunzi wenyewe katika kutekeleza dhana ya elimu ya kujitambua na kujitegemea.

9. **UMEME:**
Haitaruhusiwa kwa mwanafunzi kutumia umeme wa shule kwa sababu nyingine yoyote isipokuwa kuwasha taa tu, na kupiga pasi kwa utaratibu utakaokuwa umewekwa na wasimamizi wa bweni. Aidha ni marufuku kwa mwanafunzi kuchezea swichi au soketi.

10. **KENGELE:**
Njia ya mawasiliano shuleni ni kengele hivyo kila mwanafunzi anatakiwa kutii wito wa kengele haraka wakati inagongwa. Atakayekiuka atachukuliwa hatua za kinidhamu.

11. **BWENI:**
a. Ni marufuku mwanafunzi kubaki bwenini wakati wa masomo au shughuli zozote zilizopangwa na shule bila ruhusa ya maandishi. Atakayekiuka atachukuliwa hatua za kinidhamu.
b. Aidha ni marufuku kwa wanafunzi wawili kulala kitanda kimoja.

12. **SIMU ZA MKONONI:**
Ni marufuku kwa mwanafunzi kumiliki simu, flash, sim card, radio au kifaa chochote cha kusikiliza muziki au kuangalia sinema. Na kwa mawasiliano yoyote yale yafuate utaratibu wa ofisi ya mkuu wa shule na ni kwakupitia simu ya shule tu.

13. **USAFIRI WA SHULE (SCHOOL BUS):**
- Kwa kila mwanafunzi anayetumia usafiri wa shule anazingatia ustarabu na maelekezo anayopewa na msimamizi wa basi (Bus Guardian) na vyema mwanafunzi akishakaa kweye kiti mwingine ataheshimu utaratibu huo na unapaswa muda wote uwapo kwenye usafiri kutopiga kelele au kuongea kiswahili.
- Msimamizi wa basi atakushusha kwenye kituo husika na kuhakikisha umevuka upande wa pili wa barabara pia nakumpakia mwanfunzi asubuhi anapoelekea shuleni
- Dereva anapaswa kuendesha kwa kuzingatia sheria na taratibu za usalama wa barabarani na kutunza chombo cha usafiri.
- Sanduku la huduma ya kwanza pamoja na vifaa vyake vyote kuwepo ndani ya basi la shule

14. **KUFUTIWA USAJILI:**
Usajili wa mwanafunzi utasitishwa mara atakapofanya makosa yanayohatarisha amani na utulivu wa shule, atakapobainika kushindwa sheria za shule na za nchi yetu, na kushindwa kufuata taratibu za ratiba za shule hii ikiwa ni pamoja na kukwepa kufanya mitihani.

15. **FEDHA ZA MATUMIZI:**

Mwanafunzi wa bweni tu, kila mwanafunzi atakabidhi shuleni 25,000/- kwa kila robo mhura kwa ajili ya mahitaji madogo madogo yake binafsi. Fedha hiyo itatunzwa na matroni kwa usimamizi wa mratibu wa shule na mkuu wa shule kwa ufuatiliaji zaidi.

16. **MALIPO YA ADA:**

Ada inalipwa kwa awamu nne, awamu ya kwanza inaanza Januari, Aprili, Julai na Septemba. Malipo yote yatafanyika kupitia **KONTRO NAMBA MOJA TU** uliyopewa kwa mwaka mzima, isipokuwa michango mingine kwenye akaunti zetu za benki kama ilivyo ainishwa.

a. Kiwango ulichopangiwa kukilipia kwa awamu husika kabla ya mwanafunzi kuripoti shule hakikisha kimelipia chote kama kilivyo elekeza kwenye muundo wa ada wa mwaka

b. Ukisha kulipia kiwango hicho, unaweza kuendelea kulipia kidogo kidogo kabla ya awamu nyingine kufika na kontro namba zetu zinaruhusu kufanya hivyo.

**MUUNDO WA ADA KWA MWAKA**

**2025/2026**

| NA. | **DARASA** | **ADA** | **JANUARI** | **APRILI** | **JULAI** | **SEPTEMBA** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | CHEKECHEA NA AWALI | **400,000** | 100,000 | 100,000 | 100,000 | 100,000 |
| 2. | CHEKECHEA NA AWALI **ADA NA USAFIRI** | **800,000** | 200,000 | 200,000 | 200,000 | 200,000 |
| 3. | DARASA LA **I** HADI **VI** | **900,000** | 300,000 | 200,000 | 200,000 | 200,000 |
| 4. | DARASA LA **I** HADI **VI** **ADA NA USAFIRI** | **1,300,000** | 400,000 | 300,000 | 300,000 | 300,000 |
| 5. | MWANAFUNZI WA **BWENI** | **1,600,000** | 600,000 | 400,000 | 300,000 | 300,000 |
| 6. | ADA KWA DARASA LA MITIHANI YA KITAIFA (**DARASA LA IV - KUTWA**) | **1,500,000** | 500,000 | 400,000 | 300,000 | 300,000 |
| 7. | ADA KWA DARASA LA MITIHANI YA KITAIFA (**DARASA LA IV - BWENI**) | **1,700,000** | 700,000 | 500,000 | 300,000 | 300,000 |
| 8. | ADA KWA DARASA LA MITIHANI YA KITAIFA (**DARASA LA VII**) | **1,800,000** | 800,000 | 600,000 | 400,000 | [redacted] |

17. **MICHANGO MINGINE:**

*Vitabu, Shajala na Elimu Kwa Vitendo*

Kwa kuzingatia **Falsafa ya Shule,** Hyprlink inajitofautisha na shule nyingine kwa kujiwekea **Programu Maalum** kwa wanafunzi na wafanyakazi wake; mosi, mbali na elimu ya darasani, kuwapatia elimu ya **kujitegemea** lakini pia kuwajengea uwezo wa elimu ya **kujitambua**

| S/N | VITABU | DARASA | IDADI | SHAJALA/ELIMU KWA VITENDO | GHARAMA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | a) MATHEMATICS<br>b) KISWAHILI<br>c) ENGLISH<br>d) SST<br>e) SCIENCE<br>f) CME<br>g) KAMUSI<br>h) DICTIONARY | **VII** | 8 | Rimu **4** | [redacted] |
| | | | | Graph Pad **3** | [redacted] |
| | | | | Mathematical Sets | [redacted] |
| | | | | Dazani 1 ya Quire 3 | [redacted] |
| | | | | Holiday Package | [redacted] |
| | | | | Study Tour | [redacted] |
| | | | | Mahafali | [redacted] |
| | | | | Self-Reliance | 50,000 |
| | | | | Mitihani wa Taifa | 15,000 |
| | | | | **Jumla** | **65,000** |
| 2. | a) MATHEMATICS<br>b) KISWAHILI<br>c) ENGLISH<br>d) SST<br>e) SCIENCE<br>f) CME<br>g) KAMUSI<br>h) DICTIONARY | **V na VI** | 8 | Rimu 2 | [redacted] |
| | | | | Graph Pad **3** | [redacted] |
| | | | | Mathematical Sets | [redacted] |
| | | | | Dazani 1 ya Quire 3 | [redacted] |
| | | | | Holiday Package | [redacted] |
| | | | | Study Tour | [redacted] |
| | | | | Mahafali | [redacted] |
| | | | | Self-Reliance | 50,000 |
| | | | | Mitihani | - |
| | | | | **Jumla** | **50,000** |
| 3. | a) MATHEMATICS<br>b) SCIENCE<br>c) KISWAHILI<br>d) ENGLISH<br>e) HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI<br>f) GEOGRAPHY AND ENVIRONMENT<br>g) ARTS AND SPORTS | **IV** | 7 | Rimu **4** | [redacted] |
| | | | | Graph Pad **3** | [redacted] |
| | | | | Mathematical Sets | [redacted] |
| | | | | Dazani 1 ya Quire 3 | [redacted] |
| | | | | Holiday Package | [redacted] |
| | | | | Mahafali | [redacted] |
| | | | | Study Tour | [redacted] |
| | | | | Self-Reliance | 50,000 |
| | | | | Mitihani wa taifa | 6,000 |
| | | | | **Jumla** | **56,000** |
| 4. | a) MATHEMATICS<br>b) SCIENCE<br>c) KISWAHILI<br>d) ENGLISH<br>e) HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI | **III** | 7 | Rimu 2 | [redacted] |
| | | | | Mathematical Sets | [redacted] |
| | | | | Dazani 1 ya Quire 2 | [redacted] |
| | | | | Holiday Package | [redacted] |
| | | | | Mahafali | [redacted] |
| | | | | Study Tour | [redacted] |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | f) GEOGRAPHY AND ENVIRONMENT<br>g) ARTS AND SPORTS | | | Self-Reliance | 50,000 |
| | | | | Mitihani | - |
| | | | | **Jumla** | **50,000** |
| 5. | a) ICT SCIENCE & ARTHMETIC<br>b) KUSOMA NA KUANDIKA<br>c) READING AND WRITING<br>d) CULTURE ARTS AND SPORTS<br>e) HEALTH CARE AND NVIRONMENT | **I** na **II** | 5 | Rimu 2 | [redacted] |
| | | | | Holiday Package | |
| | | | | Daftari dazani 1 za kurasa 200 | |
| | | | | Holiday Package | |
| | | | | Mahafali | |
| | | | | Study Tour | |
| | | | | Self-Reliance | 50,000 |
| | | | | Mitihani | - |
| | | | | **Jumla** | **50,000** |
| 6. | a) ICT SCIENCE & ARTHMETIC<br>b) KUSOMA NA KUANDIKA<br>c) READING AND WRITING<br>d) CULTURE ARTS AND SPORTS<br>e) HEALTH CARE AND NVIRONMENT | **Chekechea** na **Awali** | 5 | Rimu 2 | [redacted] |
| | | | | Holiday Package | |
| | | | | Daftari dazani 1 za kurasa 200 | |
| | | | | Holiday Package | |
| | | | | Study Tour | |
| | | | | Mahafali | |
| | | | | Self-Reliance | 50,000 |
| | | | | Mitihani | - |
| | | | | **Jumla** | **50,000** |

18. **MALAZI KWA WANAFUNZI WA BWENI:**

Shule inavyo vitanda kwa kila mwanafunzi, ila anapaswa kulipia vitu vifuatavyo ambavyo vinapatikana shuleni: -

| S/N | MAELEZO YA VIFAA | GHARAMA |
|---|---|---|
| 1. | Godoro la futi 2½. linapatikana shule (DODOMA), ambalo hatarusiwa kuondoka nalo kutoka shule, ikiwa anahama au amehitimu masomo yake | 50,000/= |
| 2. | Foronya nyeusi ya ngozi (leather cover) | 30,000/= |
| **JUMLA** | | **80,000 /=** |

19. **SARE NA MAVAZI YANAYOPATIKANA SHULENI:**

| S/N | MAVAZI YA DARASANI | IDADI | TSHS |
|---|---|---|---|
| 1 | Mavazi ya Darasani Suruali /Sketi | 02@ 25,000 | 50,000 |
| | Mashati ya mikono mifupi yenye beji ya shule | 02@15,000 | 30,000 |
| | Sweta | 01@ 20,000 | 20,000 |
| | Jozi mbili za soksi | 02@5,000 | 10,000 |
| | Tai mbili | 02@ 5,000 | 10,000 |
| 2 | **Mavazi ya Michezo** | | |
| | Track suit | 03 @ 20,000 | 60,000 |
| | House Colour T-shirt | 01 @ 15,000 | 15,000 |
| | Jezi za Michezo | 02 @ 20,000 | 40,000 |
| | Gharama za kuweka alama nguo | | 20,000 |
| | JUMLA | | **255,000** |

20. **AFYA:**

Unatakiwa umwone daktari afanye uchunguzi wa afya ya mtoto, na uje na fomu iliyo ambatanishwa ikiwa imekamilika.

21. **VIFAA VYA KUNUNULIWA NA MZAZI KWA MWANAFUNZI WA BWENI:**

| Na | AINA YA VIFAA | RANGI | ALIVYOKUJA NAVYO | VINAVYO KOSEKANA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Shati mikono mifupi 2 | Nyeupe | | |
| 2 | Raba za michezo pea 1 (kulingana na mchezo anaocheza) | Nyeupe | | |
| 3 | Viatu vya Ngozi vyenye kisigino jozi 2 | Nyeusi | | |
| 4 | Blanketi moja | | | |
| 5 | Mashuka manne (4) | Light/ blue na Pink | | |
| 6 | Chandarua (4 x 6) moja | Nyeupe | | |
| 7 | Mto na foronya | Light blue | | |
| 8 | Nguo za kulalia 2 (Night dress) | | | |
| 9 | Taulo moja | | | |
| 10 | Miswaki miwili | | | |
| 11 | Dawa ya meno kubwa | | | |
| 12 | Sabuni za kuogea (Medicated or normal) vipande 10 kwa robo mhula | | | |
| 13 | Sabuni ya kufulia miche mitano(5) kwa robo mhula | | | |
| 14 | Sabuni ya unga pakti 3 kwa robo mhula | | | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 15 | Mafuta ya kujipaka | | | |
| 16 | Ndala pea mbili | | | |
| 17 | Leso nne | | | |
| 18 | Mafuta ya nywele | | | |
| 19 | Kitana | | | |
| 20 | Dawa nyeusi ya viatu kopo Kubwa | | | |
| 21 | Jozi moja ya kanga (kike) | | | |
| 22 | Brash moja ya viatu | | | |
| 23 | Shampoo (wasichana) | | | |
| 24 | Fulana (vest) nne za kuvalia ndani (wavulana) | Nyeupe | | |
| 25 | Chupi sita wasichana | Nyeupe | | |
| 26 | Chupi sita wavulana | | | |
| 27 | Vazi la kubana (Skintight nne) wasichana | Nyeusi | | |
| 28 | Sidiria | Nyeupe | | |
| 29 | Kufuli mbili imara | | | |
| 30 | Begi la kuhifadhia madaftari darasani | | | |
| 31 | Sanduku la kuhifadhia vitu vya mwanafunzi (Tranka) 1 | | | |
| 32 | Kalamu ya wino na risasi dazani moja | | | |
| 33 | Rula fupi moja 30cm | | | |
| 34 | Kichongeo (sharpener) | | | |
| 35 | Pads (wasichana) za kutosha | | | |
| 36 | Vibanio vya kubania nguo | | | |
| 37 | Mikanda ya kuvalia suruali 02 (ya ngozi) | Mweusi | | |
| 38 | Nyembe maalum zakunyolea (shaver) | | | |
| 39 | Pajama mbili kwa wavulana | | | |
| 40 | Chupa maalumu ya maji ya kunywa moja | | | |
| 41 | Sahani, Kikombe na Kijiko | | | |
| 42 | Viatu vya wazi vya ngozi (Sandals) jozi moja vyenye mikanda zaidi ya miwili inayofunga mbele na nyuma) | Nyeusi | | |
| 43 | Ndoo ya kuogea moja na beseni moja | | | |
| 44 | Picha Passport size 2 | | | |
| 45 | Hijabu (wasichana wa kiislam tu). Mitandio hairuhusiwi. | Nyeupe 2 | | |

## UTARATIBU WA KUJIUNGA NA SHULE YA HYPERLINK

Sifa Muhimu kwa mwanafunzi kujiunga na shule yetu ni lazima awe amefanya usahili na kumbukumbu zake zimehifadhiwa vizuri kwaajili ya rejea. Shule yetu ni shule ya Mchanganyiko (Wavulana na Wasichana) Kwa kipindi chote mwanao awapo shuleni atapaswa kudumisha nidhamu, kusoma kwa bidii, kutii sheria, kanuni na taratibu za shule.

## MUUNDO WA USAILI

1. **MAADILI BINAFSI:**
   Mwanafunzi atafanya mtihani utako mpima maadili yake binafsi

2. **KUJITAMBUA:**
   Mwanafunzi atafanyishwa jaribio la kubainisha uwezo wake kwenye kujitambua

3. **STADI ZA KAZI:**
   Mtihani wake hapo unaenda kupima anastadi zipi za kazi au Maisha ili itusaidie shule namna bora ya kumtengenezea utaratibu wa mafunzo yake ya stadi za kazi awapo shuleni.

4. **MTIHANI WA KUPIMA UMAHIRI:**
   - Kusikiliza, Kufikiri, Kuandika, Kusoma, na Kuhesabu

5. **MTIHANI WA DINI KWA IMANI YAKE:**

   Mwanafunzi atapatiwa Mtihani wa dini kulingana na Imani yake kwa mujibu wa mzazi alivyoweza kujaza taarifa muhimu za mwanae.

## TAARIFA MUHIMU ZA MWANAFUNZI

1. **Jina la Mwanafunzi**
   Jina la Kwanza ............................................Jina la Kati...................................
   Jina la Ukoo................................................Tarehe ya Kuzaliwa..........................
   Jinsia...........................Wakiume/ wakike, Shule Alikokuwa akisoma....................
   Darasa Analotakiwa kujiunga nalo.......................... Imani Yake.........................
   Kutwa/ Bweni.....................................................................................................

2. **Jina la Mzazi/ Mlezi**
   Jina la kwanza..................................... Jina la Ukoo...........................................
   Namba ya Simu .................Barua pepe...............................Kazi .............
   Unapoishi, Mtaa.........................................Kata......................................
   Wilaya...............................................Mkoa...........................................
   Shughuli za kiuchumi.........................., ..................................................,
   Shughuli hizi muhimu kwa shule kuzijua ili kuweza kumuendeleza mwanao kwenye misingi inayoanzia nyumbani kwenye familia.

3. **Afya ya Mwanafunzi**
   Taja taarifa muhimu ya kitabibu kuhusu mwanafunzi...................................
   Taja chanjo ambayo mwanafunzi amepatiwa ..........................................

4. **Kwa dharula yoyote ile, shule inaweza kuwasiliana na**:
   Jina la kwanza....................................... Jina la Ukoo...........................................
   Namba ya Simu .................. Barua pepe.............................................
   Kazi...........................Mahusiano yake na Mwanafunzi...............................
   Mahali, Mtaa...........................................Kata....................................
   Wilaya.........................................Mkoa.............................................

5. **Viambatanisho vya Mwanafunzi**
   a. Cheti cha Kuzaliwa
   b. Picha ya Mwanafunzi (**Pass Port Size, Back Ground Color-Blue**)
   c. Cheti cha Uhamisho Toka shule anayohama

6. **Vigezo na Masharti**
   - Takwa la shule kwa kila Mwanafunzi anayejiunga nasi ni lazima awe amefuzu majaribio na usaili ili asajiliwe na shule
   - Nimekubali Vigezo na Masharti ya shule na ninathibitisha pasina shaka kuwa taarifa zilizotolewa hapo juu ni za kweli

### UTHIBITISHO WA MZAZI/MLEZI:

Nimesoma na kuelewa sheria, taratibu na kanuni pia ninakubali mtoto wangu adhibitiwe kwa sheria hizi.

Jina la Mzazi/Mlezi..............................................................................

Sahihi.........................................Tarehe ..............................................

Jina la Mwanafunzi......................................................................

Sahihi.........................................Tarehe ..........................................

## Maoni/Mapendekezo ya Mzazi